

**HOTUBA YA MHE. MKUU WA MKOA WAKATI WA UZINDUZI
WA DCC YA WILAYA YA KINONDONI TAREHE 07/11/2008**

**Ndugu Mwenyekiti,
Ndugu Mstahiki Meya,
Ndugu Mkurugenzi,
Ndugu Wajumbe.**

Natoa shukrani kwa kunikaribisha katika uzinduzi wa kikao cha kwanza cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya. Aidha, natoa pongezi kwa kuwa Wajumbe wa District Consultative Committee ya kwanza katika historia ya Wilaya ya Kinondoni.

Kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho Na.13 ya 2006, Kamati hii inaundwa. Yako majukumu makuu saba ambayo mmepewa. Nitazungumzia yanayohusu:

- a) Kupokea taarifa za mipango ya maendeleo na kutoa ushauri kwa Halmashauri;
- b) Kuhakikisha Halmashauri zimetekeleza majukumu na shughuli za maendeleo
- c) Kuhakikisha Halmashauri zinatekeleza kwa ufanisi maamuzi yanayotokana na vikao vyao.

Ndugu Wajumbe,

Kwa nini majukumu haya yametolewa kwa Manispaa zetu, ni kwa sababu Manispaa zetu ndivyo vyombo vikuu vya utekelezaji.

- Vina Watumishi
- Vina nyenzo
- Vinapewa fedha za ruzuku
- Vinakusanya mapato kutoka vyanzo vyao.

Katika kutekeleza majukumu haya matatu tunayo matatizo:

- **Kuhusu taarifa:**

Mara nyingi hazitoki kwa wakati, na zikitoka si sahihi. Yote hii inatokana na watu kutojua nini kinaendelea. Wapo maofisini na Watendaji hawako kwenye Vituo vya kazi. Wanaonekana wakati wa ziara za Viongozi. Mbaya zaidi ni kwamba umejengeka utamaduni wa kudai posho kwa hata kazi za kawaida zisizostahili kulipiwa posho.

- **Kuhusu Utekelezaji:**

Upo udhaifu mkubwa sana wa usimamizi, matokeo yake ni uduni wa ubora wa kazi. Kasoro kubwa hapa ni kutoteremsha mamlaka na madaraka kwenda ngazi ya chini ya L.G. (Mitaa na Kata): Pelekeni fedha, nyenzo (D by D).

- **Kuhusu maamuzi ya Vikao:**

Hili nalo ni eneo ambalo upo udhaifu mkubwa kupindukia. Maazimio mengi sana, lakini hakuna utekelezaji: k.m. kelele, gereji bubu, grocery, uchafu, Omba Omba (kila wakati vikao, hivi havitaondoa kero). Vikao vina maana pale tu unapokuwepo utekelezaji wa maazimio, vinginevyo ni kupoteza fedha za Umma kupitia posho.

Ndugu Mwenyekiti,

DCC yako nategemea iishauri Manispaa ijijengee uhalali wa kuwepo mbele ya Umma kwa kufanya yafuatayo:

- Ishughulikie kero ya miundo mbinu: mifereji ya kutoa maji barabarani, itengeneze barabara mara uharibifu unapotokea na isikie kilio cha watu kuhusu kuta zilizojengwa katika mikondo ya asili ya maji. Serikali Kuu itaendelea kushirikiana na Manispaa zote (ndiyo mwajibikaji wa mwisho kwa wananchi): k.m. Ubungo – Kigogo – Jangwani, Kilwa, Kawe, Old Bagamoyo.
- Ishughulike tatizo la uchafu uliokithiri. Hili si la Operation, ni la kazi za kila siku. Viongozi wa ngazi zote hadi pale Mtaani washiriki kusimamia sheria zitumike kuhimiza usafi.
- Ishughulikie kero zinazowagusa watu tena kwa haraka na siyo kwa maneno na kuagizana. Kuagiza kufuatiwe na kufuatilia kuona kama agizo limetekelezwa.
- Ihakikishe inawashirikisha wananchi katika mipango mbalimbali inayowahusu katika kupanga na kuchangia utekelezaji. Udhaifu mkubwa sana unajitokeza katika ujenzi wa Shule za Sekondari.

- Iondokane na udhaifu katika kuhakikisha mafanikio yanayopatikana yanakuwa endelevu (k.m. zoezi la Machinga na Omba Omba).
- Iondokane na unyonge wa kutokupokea ushauri. Isipofanya hivyo, basi nyinyi mtakuwa mnashauri, lakini ushauri hauzingatiwi. Huu si wakati wa umimi au nani mkubwa. Tukumbuke sisi wote ni Watumishi wa watu, tuwatumikie. Tusiwakwamishe kwa sababu zetu za ubinafsi.

Ndugu Mwenyekiti,

Pamoja na kujadili agenda zenu mlizojipangia, nashauri mtafakari yafuatayo ili muishauri mamlaka husika ipasavyo:-

- Rangi za Taxi na Taxi bubu
- Usafiri wa Wanafunzi
- Kutenga maeneo mahsusi ya biashara ndogo ndogo jioni
- Mfuko wa Elimu na ujenzi wa Shule za Sekondari.

Mwisho, kumbukeni mnajenga historia. Mnataka mkumbukwe kwa lipi? Hilo ndilo swali ninalotaka muwe mnajiuliza kila siku. Mkiwa makini jibu mtakalopata ni kwamba mtakumbukwa kwa kuwa na utumishi uliotukuka na si ujuzi wa kujenga hoja kwenye vikao au kuwa mbishi kwa kila linalojadiliwa. Watu wanataka kuona vitendo, na kwa hilo watatuheshimu.

Baada ya kusema hayo sasa natamka kwamba Kamati ya Ushauri ya Wilaya nimeizindua rasmi.